TANGAZO LA SERIKALI NA 836 LA TAREHE 02/10/2020

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**SURA YA 288**

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 89*

**SHERIA NDOGO ZA HIFADHI YA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2020**

## SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"eneo la hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria

Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote itakayotamkwa na Halmashauri kuwa ni hifadhi ya mazingira;

Sura 191

Sura 191 “kibali cha hifadhi ya Mazingira” maana yake ni kibali kinachotolewa na Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa;

Sura 323 “kiwanda” maana yake ni jengo, majengo au eneo ambapo vitu au bidhaa zinatengenezwa au kuzalishwa.

Sura 191 “maji” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa

Mazingira;

“maji taka” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira;

“mazao ya misitu” maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu kifungu cha 2;

Sura 323

“mazingira” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191 “Halmashauri “ maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya;

Sura 191 “Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Sura 191

“Mfugaji” maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

Sura 191

Sura 191 “Mifugo” maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu;

Sura 191

“Misitu” maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au
Sura 191 iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu

ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"Taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka ngumu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka za viwandani" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"uchafu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 133(5) cha Sheria ya usimamizi wa Mazingira;

"uchafuzi wa mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"udongo"maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"vitu hatari" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

## SEHEMU YA PILI: UFUGAJI NA HIFADHI YA MAZINGIRA

*Wajibu wa mfugaji*

4. Chini ya Sheria Ndogo hizi kila mfugaji;
   (a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyo amriwa na Halmashauri;
   (b) atahakikisha kuwa anatunza au kulaza mifugo katika nyumba au sehemu ya nyumba ambayo haitumiki kwa makazi ya binadamu;
   (c) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayo onyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo.

*Masharti kwa Mfugaji*

5. Ni marufuku kwa mfugaji;
   (a) Kusafirisha mifugo kwa kuiswaga au kupitisha barabarani;
   (b) Kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja

hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;

(c) Kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(d) Kufuga mifugo mingi Zaidi ya idadi ya mifugo iliyoainishwa katika kibali kilichotolewa na Halmashauri; na

(e) Kuingiza mifugo ndani ya eneo la Halmashauri kwa lengo la kulisha, kunywesha au kufanya biashara bila kibali na bila kufuata utaratibu uliowekwa na Halmashauri.

*Kudhibiti mifugo inayozurua hovyo*

6 (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji kuhakikisha kwamba:-

(a) mifugo yake inafungiwa na kuhudumiwa ndani ya eneo lake;

(b) mifugo yake haiharibu mazingira; na

(c) mifugo yake haizururi hovyo mitaani.

(2) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakao onekana unazurura hovyo au kulishwa katika maeneo yasiyoruhusiwa katika eneo la Halmashauri

(3) Mfugo wowote utakao kamatwa utalipiwa faini kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi

(4) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya kipindi masaa ishirini na nne (24) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama

(5) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo pindi itakapoona kuna umuhimu wa kufanya hivyo na kutoa elimu juu ya ufugaji bora na endelevu usioharibu mazingira.

**SEHEMU YA TATU:**
**KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI**

*Taratibu za Kilimo Sura ya 113*

7(1) Mtu yeyote atakayetaka kufanya shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kwa kuzingatia Kalenda ya Kilimo ya Halmashauri na Sheria ya Ardhi na Sheria nyingine zozote.

(2) Itakuwa halali kwa Halmashauri kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi

*Masharti kwa Mkulima*

8 Itakuwa ni marufuku kwa mkulima au mtu yeyote;

(a) Kufanya shughuli za kilimo cha mazao marefu ya zaidi ya futi tatu katika eneo lote la Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.

(b) Kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, Mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa Kilimo.

(c) Kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

*Uchimbaji na Usafirishaji wa Madini ya Ujenzi, Ufyatuaji na uchomaji wa tofali*

9. (1) Mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli za utafiti au uchimbaji wa mchanga, kokoto, mawe, kifusi, udongo, ufyatuaji na uchomaji wa tofali ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kufuata taratibu kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga, kokoto, mawe, udongo, kifusi na au kufyatua tofali katika maeneo ndani ya Halmashauri au maeneo yasiyoruhusiwa kama vile maeneo ya makazi ya watu, miteremko, makorongo, maeneo ya hifadhi, kandokando ya mito au ndani ya mto, pembezoni mwa barabara, mabwawa na maeneo ya ardhi oevu isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(3) Mtu yeyote anayefanya shughuli za ufyatuaji na

uchomaji matofali katika eneo la Halmashauri atatakiwa kulipa ada au ushuru kwenye Halmashauri kama inavyoonesha kwenye Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

*Kibali cha kuchoma moto*

10. (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa kuchoma moto isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri.

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(3) Muda unaoruhusiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.

*Uhifadhi wa Ardhi*

11. Itakuwa ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti na kuendelea kutoharibu mazingira ili kuwezesha uoto urudi katika hali yake ya kawaida.

*Ujenzi Holela*

12. Mtu yeyote hataruhusiwa kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo ambalo Halmashauri imetangaza kuwa eneo la Hifadhi.

## SEHEMU YA NNE:
## HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

*Wajibu wa Kulinda Vyanzo vya Maji*

13. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu ndani ya Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Mwidhiniwa.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote;

(a) kuishi, kulima, kukata miti, kuchunga kufuga, au kunywesha mifugo, kufyatua tofali au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote eneo lililotangazwa kuwa eneo la hifadhi au chanzo cha maji, au mto au kingo ya mto, kisima au bwawa;

(b) kumiliki eneo la chanzo cha maji kilichopo

ndani ya Halmashauri, au

(c) kupanda ndani ya mita sitini mmea au sehemu ya mmea uwe wa asili au usio wa asili ambao husababisha kukausha vyanzo vya maji.

*Uchafuzi wa vyanzo vya maji*

14. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, visima, mifereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine hai.

**SEHEMU YA TANO:**
**UHIFADHI WA UOTO WA ASILI NA MISITU**

Wajibu wa kupanda miti, kuhifadhi na kulinda uoto wa asili na hifadhi ya misitu.

15. (1) Kila mtu anayeishi ndani ya Halmashauri ana wajibu wa kutunza, kulinda na kutoharibu uoto wa asili na hifadhi za misitu.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa ardhi kupanda na kuhifadhi miti isiyopungua mitano (5) kulingana na mazingira ya eneo lake.

(3) Mmiliki yeyote wa kiwanja sharti aoneshe kuwa katika ramani yake ya kiwanja kuna miti isiyopungua mitano wakati anaomba kibali cha ujenzi.

(4) Halmashauri itapanga siku moja au zaidi kwa kila mwaka kwa ajili ya kupanda miti, na wakazi wote wa Halmashauri watahamasishwa kushiriki katika zoezi hilo.

(5) Kila asasi na taasisi zilizomo ndani ya Halmashauri zitahakikisha kwamba:

(a) zinapanda na kutunza miti katika maeneo yaliyo chini ya uangalizi wao;

(b) zinashiriki vema katika shughuli za kupanda miti na kuhifadhi mazingira pale watakapotakiwa kufanya hivyo;

(c) zinashirikiana na Halmashauri katika kukuza weledi, kuhamasisha na kuwezesha wananchi juu ya njia bora za usimamizi na utunzaji wa uoto wa asili, misitu na mazingira;

(d) zinatoa taarifa mara moja kwa Halmashauri pale

inapobainika kuwa kuna uharibifu wowote wa uoto wa asili, misitu na mazingira kwa ujumla katika eneo lolote ndani ya Halmashauri.

Kuchoma au kusababisha moto.

16. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto msitu, uoto wa asili au nyika kwa namna yoyote ile ndani ya eneo la Halmashauri ya Jiji bila idhini ya Afisa Mwidhiniwa.

(2) Ni jukumu la Afisa Mtendaji wa Kata na au Mwenyekiti wa Mtaa kuhamasisha au kutoa amri kwa wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo.

Kukata mti au miti.

17. Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata au kuvuna mti, sehemu ya mti au miti kwa ajili ya matumizi yoyote ndani ya eneo la Halmashauri ya bila idhini ya Halmashauri.

## SEHEMU YA SITA:
## TAKA NGUMU NA MIMINIKA

*Utupaji wa taka ngumu*

18. Ni wajibu wa kila Mtu ndani ya eneo la Halmashauri kuwa na chombo chenye mshikio na mfuniko chenye ukubwa usiopungua lita 20 kwa ajili ya kuhifadhia takataka.

*Utunzaji wa mifereji ya maji ya mvua*

19. (1) Mifereji ya maji ya mvua daima inapaswa kuwa safi muda wote kwa madhumuni yaliyoifanya ijengwe na hivyo ni wajibu wa mmiliki, msimamizi, mtumiaji au mpangaji wa eneo lililo karibu na mfereji wa maji ya mvua kufanyia usafi eneo hilo.

(2) Itakuwa ni wajibu wa mmiliki, msimamizi, mtumiaji au mpangaji wa eneo lililo karibu na mfereji wa maji ya mvua kufanyia usafi eneo hilo.

*Uendeshaji wa viwanda*

20. Itakuwa ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuwa na kibali cha mazingira

*Kamati au*

21. (1) Halmashauri itaunda kamati au vikundi vya

*vikundi vya Mazingira*

mazingira kwenye kila Kata na Mtaa itakayojihusisha na usimamizi wa mazingira kwenye kila Kata na Mtaa husika.

(2) Kamati au vikundi vilivyoundwa katika kifungu kidogo cha 21(1) zitashirikiana na Askari mgambo wa Halmashauri kupita na kukagua usafi wa nyumba kwa nyumba na maeneo yote ya Halmashauri na ikibaini ukiukwaji wa Sheria Ndogo hizi kamati zitakuwa na mamlaka ya kutoza faini za papo kwa papo ya kiasi kisichozidi laki tatu kwa kila kosa, iwapo mkosaji atakataa kuilipa faini atashitakiwa mahakamani.

(3) Mapato yatakayo kusanywa katika kifungu kidogo cha (2) cha Sheria Ndogo hizi yatagawanywa kama ifuatavyo;

(a) Asilimia 20% itakuwa ni posho ya Askari mgambo waliohusika;

(b) Asilimia 50% itabaki kwa matumizi ya Ofisi ya Kata au Mtaa; na

(c) Asilimia 30% itaingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri

Utupaji wa maji taka na taka miminika katika eneo zilipozalishwa.

22. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutiririsha maji taka toka nyumbani, kiwandani au sehemu nyingine na kuyaelekeza ardhini, mtoni, barabarani, au kwenye mifereji ya kutiririshia maji ya mvua.

(2) Kila mmiliki wa nyumba ya kuishi au eneo la biashara, nyumba ya burudani au kiongozi wa Ofisi ya Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali atahakikisha kuwa anakuwa na mfumo bora wa kuhifadhi taka miminika ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa anachimba na kujengea mfumo wa kutunzia maji taka au taka miminika au kuunganisha kwenye mfumo wa maji taka.

(3) Mtu yoyote au taasisi ambayo haijaunganisha maji taka kwenye mfumo wa maji taka itatakiwa kukodi magari ya kunyonya maji taka na kulipa ushuru kama inavyoonesha kwenye Jedwali la tatu la Sheria ndogo hizi.

*Wajibu wa kuunganisha mfumo wa Maji taka*

23. (1) Kwa maeneo ambayo mfumo wa maji taka umepita

ni wajibu wa kila mkazi, taasisi au kiwanda kuunganisha maji taka kwenye mtandao wa maji taka.

(2) Endapo mtu yeyote, taasisi au kiwanda kabla ya kutiririsha maji taka kwenye mfumo wa maji taka wa umma (public sewer) watatakiwa kuwa na mitambo ya kusafisha na kutakasa maji taka hayo kabla ya kuyatiririsha katika mtandao kwa kuzingatia viwango vilivyokubalika kwa mujibu wa kanuni za ubora wa maji.

(3) Itakuwa ni kosa kuhujumu mfumo wa maji taka kwa kuiba, kuvunja au kuharibu kwa namna yoyote ile miundombinu ya mfumo wa maji taka.

*Utengenezaji na uoshaji wa vyombo vya moto*

24 (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza au kuosha magari, bajaj, pikipiki (bodaboda) katika maeneo ya vituo vya mabasi, barabarani, kando ya mito na maeneo au katika hifadhi mazingira cha Halmashauri.

(2) Mtu atakayepewa kibali cha hifadhi ya mazingira atatakiwa kuhakikisha mambo yafuatayo:

(a) kutumia maji safi ya bomba au kisima;
(b) kusakafia eneo lote litakalotumika kwa shughuli za kuoshea magari;
(c) kuwa na mfumo bora wa maji taka ikiwa ni pamoja na mifereji iliyojengewa kupitisha maji taka hadi kwenye shimo sanifu la maji taka au kuunganisha kwenye mfumo wa maji taka;
(d) kuwa na mfumo bora wa kutenganisha vilainishi au girisi na maji taka mengine;
(e) kuwa na chombo bora cha kuhifadhia taka ngumu;
(f) Kuwa na choo bora na kukitumia;

*Udhibiti wa taka hatari mahali zinapozalishwa*
*Sura 191*

25. Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda, eneo la biashara au eneo au sehemu yoyote ambapo taka hatari huzalishwa anatakiwa kuhakikisha mambo yafuatayo:

(a) Kuna kuwa na hewa ya kutosha na mitambo inayotoa gesi taka hatari inafungwa kuzuia uchafuzi

wa hewa na kuhakikisha vifaa hivyo vinakidhi viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

(b) kuhakikisha kuwa taka hatari miminika zinatakaswa kabla ya kupelekwa kwenye mfumo wa maji taka au kuhifadhiwa sehemu iliyothibitishwa na Halmashauri;

(c) kuwa na kifaa maalumu cha kuhifadhia taka hatari na kuhakikisha zinatenganishwa na aina nyingine ya taka zisizo hatari kabla ya kutupwa kwa utaratibu atakaopewa na Halmashauri; na

(d) kuhakikisha kuwa watu wote wanaohusika na kuhifadhi, kutumia au kusafirisha taka hatari wanavaa vifaa kinga.

*Kuzuia umwagaji wa taka hatari, kemikali, mafuta n.k*

26. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote, taasisi, kampuni au kiwanda kumwaga taka hatari, kemikali, mafuta au mchanganyiko wenye mafuta kwenye eneo lake au eneo lolote la ardhi au maji au sehemu yoyote ya mazingira isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka Halmashauri

(2) Mtu yeyote aliyepewa kibali cha kutupa taka hatari, mafuta au mchanganyiko wa mafuta kwenye sehemu yoyote atatakiwa kuhakikisha kuwa anatakasa taka hatari kabla ya kumwaga kwenye eneo lililoruhusiwa.

(3) Mbali na adhabu ya jumla inayotolewa chini ya Sheria Ndogo hii mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu hiki anaweza kuamrishwa na Mahakama:

(a) Kulipa gharama za kuondosha takataka pamoja na gharama zozote ambazo Serikali au Wakala wa Serikali wamegharamia katika urejeshwaji wa hali ya mazingira yaliyoharibika kutokana na umwagaji; na

(b) Kulipa gharama za walioathiriwa kwa njia ya umwagaji, ukarabati, urejeshaji katika hali ya awali au fidia kama itakavyoamriwa na mahakama.

*Udhibiti wa vyombo vitoavyo kelele kubwa*

27.

## SEHEMU YA SABA

## KELELE NA MITETEMO

(1) Itakuwa ni marufuku kupitisha vyombo vya usafiri wa barabara vitoavyo sauti kubwa katika maeneo maalumu na yanayohitaji utulivu ambayo ni hospitali, mashuleni, na Ofisi za Taasisi mbalimbali.

(2) Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kibiashara kama vile muziki, mihadhara, minada na matangazo yoyote ya kibiashara kwa kutumia vipaza sauti atatakiwa kupata kibali cha Halmashauri na kulipa ada ya Tsh. **50,000** kwa siku na Tsh.**300,000** kwa mwezi.

(3) Mtu yeyote aliyepewa kibali cha matangazo na mikutano atatakiwa kufanya matangazo au mikutano hiyo kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kwenye kanuni za udhibiti wa kelele na mitetemo za mwaka 2011.

(4) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki, msimamizi au mpangaji wa kumbi za starehe kuhakikisha kwamba kumbi zote zinazojengwa katika eneo la Halmashauri lazima ziwe na kidhibiti sauti (sound proof)

## SEHEMU YA NANE:

## MAKOSA NA ADHABU

*Makosa*

28. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;

(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(b) atasafirisha mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(c) ataingiza mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;

(e) atalima mazao marefu ya zaidi ya futi tatu katika maeneo ya Halmashauri

(f) atakiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini na udongo katika maeneo yasiyoruhusiwa;
(g) atakiuka masharti ya kuhifadhi ardhi;
(h) ataharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji;
(i) atabainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine;
(j) atatupa hovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa;
(k) ataosha magari katika maeneo yasiyoruhusiwa;
(l) atatiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai;
(m) atafuga mifugo bila kufuata kibali na kanuni bora za ufugaji;
(n) kuacha mifugo inazurula hovyo;
(o) ataendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji.

*Adhabu*

29. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

*Kufililisha kosa*

30. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoelekezwa katika Jedwali na Nne la Sheria Ndogo hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 6(3))*

**VIWANGO VYA FAINI KWA MIFUGO ILIYOKAMATWA**

| NA | AINA YA MIFUGO | IDADI YA MIFUGO ILIYOKAMATWA | VIWANGO VYA FAINI KWA KILA MFUGO ULIOKAMATWA VYA ZAMANI | VIWANGO VYA FAINI KWA KILA MFUGO ULIOKAMATWA VYA SASA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Kwa kila Ng'ombe aliyekamatwa | 30,000/= | 50,000/= |
| 2. | Punda/farasi | Kwa kila Punda aliyekamatwa | 20,000/= | 40,000/= |
| 3. | Mbuzi | Kwa kila Mbuzi aliyekamatwa | 20,000/= | 30,000/= |
| 4. | Kondoo | Kwa kila Kondoo aliyekamatwa | 20,000/= | 30,000/= |
| 5. | Nguruwe | Kwa kila Nguruwe aliyekamatwa | 20,000/= | 20,000/= |
| 6. | Paka/ mbwa | Kwa kila mnyama aliyekamatwa | 20,000/= | 30,000/= |

## JEDWALI LA PILI

*(Chini ya Kifungu cha 9(3))*

ADA NA USHURU KWA SHUGHULI ZA UFYATUAJI MATOFALI

| | SHUGHULI | ADA/USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ufyatuaji na uchomaji matofali kwa matumizi ya kawaida | 30,000 kwa tofali zisizozidi 10000<br><br>50,000 kwa tofali zisizozidi |

| | | |
|---|---|---|
| | | 30000<br><br>100,000 kwa tofali zisizozidi 50,000 |
| 2. | Ufyatuaji na uchomaji matofali kibiashara | 300,000 kwa mwaka |

## JEDWALI LA TATU

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 22 (3))*

GHARAMA ZA KUNYONYA MAJI TAKA KWA KUTUMIA MAGARI YA HALMASHAURI

| NA. | AINA YA HUDUMA | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1. | Kuzibua mtandao wa maji taka majumbani (si katika shughuli binafsi)<br><br>a) Maeneo ya viwanda<br>b) Maeneo ya biashara<br>c) Maeneo ya makazi<br>d) Taasisi | 20,000<br>15,000<br>10,000<br>15,000 |
| 2. | Uondoaji maji taka shimoni<br><br>(a) Maeneo ya viwanda kwa safari<br>a) Maeneo ya biashara kwa safari<br>b) Maeneo ya makazi kwa safari<br>c) Taasisi kwa safari<br>d) Ada za umbali nje ya mipaka ya Jiji kwa kilomita kwenda na kurudi | 130,000<br><br>120,000<br><br>100,000<br><br>120,000<br><br>6,000 |

**JEDWALI LA NNE**

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 30)*

**HATI YA KUKIRI KOSA**

Mimi ………………………………………… nakiri mbele ya …………………………………… ambaye ni Mkurugenzi, kwamba, mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi ninachodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe …… ya mwezi …………… mwaka …………
Jina……………………..…………………………
Saini……………
Mbele ya:

Jina………………………………………………….
Cheo ………………………………………………..
Saini ………………

Muhuri wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya Umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio la kikao cha Mkuatano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10/06/2020 na kubandikwa mbele ya;

LS

SAAD A. MTAMBULE
*Kaimu Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**GIBSON J. MWAKALIBULE**

*Mwenyekiti wa Mkutano*

*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**NAKUBALI**

DODOMA SELEMANI S. JAFO

05 Agosti, 2020 *WN OR-TAMISEMI*

DODOMA